Tafuteni Kwanza Ufalme Wa Mungu

na

Ellis P. Forsman

Tafuteni Kwanza Ufalme Wa Mungu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

“Tafuteni Kwanza Ufalme Wa Mungu”

Mat. 6:24-34

Yesu alitoa maelezo haya yaliyo rekodiwa katika sura ya 6 ya Mathayo kwamba tunapaswa kumwamini na tusiwe na wasiwasi kuhusu vitu katika maisha haya.

- Mat. 6:25, “*Kwa sababu hiyo nawaambieni, nsisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?*
- Mat. 6:31, “*Msisumbuke, basi, mkisema tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini?*”
- Mat. 6:33, “*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*”

Ni nani anyeishi kwa ajili ya haya? Nani anayeyatenda? Hasa tunapofundishwa kuwa na bidii.

Rum. 12:11, “*Kwa bidii si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana.*”

Tunafundishwa kupata kwa wakati ujao. Mit. 6:6, “*Ewe mvivu, mwendee chungu, zitafakari njia zake ukapate hekima.*”

Hiki ndicho ambacho Yusufu alifanya Misri. Alitafsiri ndoto ya Farao na kusema kutakuwa na miaka 7 ya chakula kingi ikifuatiwa na miaka 7 ya njaa, na akaonyesha kwamba wanapaswa kuweka pembeni kutoka katika miaka 7 ya chakula kingi, ili kutafuta kwa ajili ya miaka 7 ya njaa.

Tatizo linakuja kwamba tunapokuwa na wasiwasi na kufanya maamuzi yasiyo sahihi, bila kumuweka Mungu kwanza katika maisha yetu.

Hatupaswi kuwa na wasiwasi kuhusu siku zijazo. Tunafanya kile tuwezalo na tusijali kuhusu mengineyo.

Katika kifungu chetu cha maandiko, Yesu anahitaji kwamba tuweke ufalme wa Mungu na kazi ya Mungu juu ya vitu vyote katika maisha. Kifungu hiki kiasili inajigawa yenyewe katika sehemu mbili katika Mat. 6:33:

- Jukumu kuu linahitajika – “*…tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; …*”
- Ahadi yenye hisani imewekwa – “*… na hayo yote mtazidishiwa.*”

Jukumu kuu linahitajika – "... *tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; …*"

Kifaa cha kutafuta.

"*ufalme wa Mungu*"

Hiki ni nini? Ambacho Yesu anatuambia. Yohana 18:36, "*Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania, nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa.*"

Sio ya ulimwengu huu kwa sababu haukutokana na ulimwengu huu, bali ulitoka mbinguni.

Sio sawa na ufalme wa kidunia. Haihusiani na maeneo, mipaka, au nchi. Hakuna mji kuu au makao makuu ya kufikia. Makao yake makuu yako mbinguni, na Yesu ndiye Mfalme wake mkuu.

Rum. 14:17, "*Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.*"

Ukristo haupo katika tamaa za wanadamu kwa ajili ya vitu ambavyo vipo katika maisha haya. Luka 17:21, "*Wala hawatasema, tazama upo huku, au kule kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu.*" Hiyo ni, kutokea kwake hakuwezi kutazamwa kwa hisia tano.

Ufalme wa Mungu hauwezi kuja na muonekano wa kifalme wa dunia au serikali. Ufalme wa Mungu unakaa ndani ya wafuasi wa Kristo.

Yoh. 3:5, "*Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia Ufalme wa Mungu.*"

Ni uzazi wa kiroho. Yesu alikuja kutimiza haki yote.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba katika Mat. 6:10, "*Ufalme wako uje. Mapenzi yako yafanyike duniani, kama huko mbinguni.*"

Wakati haya yalipokuwa yakisemwa ufalme ulikuwa bado haujaanzishwa, lakini tunayo leo. Ufalme wa Mungu ni utawala wa Mungu katika nyanja zote za shughuli za binadamu; hivyo uzuri huu hauja gundulika katika sehemu yote ya maisha haya leo.

"na haki yake"

Haki ni tunda la utawala wa Mungu katika moyo. Zaburi 119:172, "*Ulimi wangu na uiimbe ahadi yako, maana maagizo yako yote ni ya haki.*"

Yesu hatuambii tu kutafuta haki, bali haki **Yake**. Haki yo yote tuliojitengenezea haina uthamani wowote.

- Isa. 64:6, "*Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi, sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa kama upepo uondoavyo.*
- Rum. 10:3, "*Kwa maana wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.*"

Haki Yake ni ya nguo safi yote na haita haribika. Fil. 3:8-10, "*Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi kwa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani; ili nimjue yeye na uweza, wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake.*"

Paulo alisema kuwa haki ya Agano La Kale ili kuwa ni kuwekwa pembeni. Imani uja kwa kusikia neno la Mungu.

Je ulishawahi kujiuliza kwamba kwa nini Yesu alibatizwa? Mat. 3:13-17, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili ambatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akakubali. Naye Yesu alipotokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.*"

Hivyo, tunapaswa mkuruhusu Mungu awe na mamlaka juu yetu; atawale pasipopingamizi.

Mpangilio wa utafutaji – "*tafuteni Kwanza*".

"Kwanza" inamaanisha kwamba kuna vitu vingine ambavyo tunavitafuta, lakini vinapaswa kutothaminishwa (shushwa kiwango). "Kwanza" inamaanisha kwamba kuna mengine.

Hatupaswi kuutafuta ufalme wa Mungu kwa kukataa majukumu yetu ya dunia; hataivyo, hatuwezi kuruhusu majuku haya ya kidunia kuingilia majukumu ya mbinguni.

Bwana wetu haitaji kwamba tuwe bila mawazo kuhusu vitu vya maisha haya.

1 Tim. 5:8, "*Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.*"

Roho ambayo haijali na kuwajibika huondolewa katika roho wa kweli wa Ukristo. Rum. 12:11, "*Kwa bidii si walegevu, mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana;*"

Mkristo wa kweli anachukia uchafu kama anavyochukia ulevi, na kukimbia mambo ya kipuuzi kama anavyo kimbia kutoka katika zinaa.

Bali tunapaswa kuweka vitu vya kwanza nambari moja , na tusiruhusu kazi ya Mungu katika maisha yetu yatingwe na mambo ambayo hayana umuhimu.

Hatuwezi kuruhusu kazi zetu, masomo ya chuo, michezo, burudani, au kitu chochote kile kije kati yetu na huduma yetu kwa Mungu. Lazima tumuweke awe wa kwanza katika kila jambo tunalofanya.

Ujuzi wangu wa kuomba kazi katika shamba la Real Estate. Niliombwa kufanya kazi siku ya juma pili. Niliambiwa, "Hufai katika kazi hii". Nikajibu, "Hapana hii kazi sio ya kwangu."

Ujuzi wangu wa kuomba kazi katika Kiwanda Cha Ndege. Niliwaambia nilikuwa napenda kufanya kazi siku yo yote ya wiki na muda wo wote katika siku, isipokuwa niliitaji kuwa kanisani jumapili asubuhi. Tulikubaliana katika hili na barua ya makubaliano iliwekwa katika faili langu kwamba sitahitajika kazini siku za juma pili asubuhi. Walijaribu hili mara moja tu. Nikawakumbusha makubaliano yetu, na wakanigeuka wakitaka nifanye kazi jumapili moja asubuhi. Nimefanya kazi masaa mengine yote ya siku isipokuwa siku ya jumapili asubuhi.

Kwa nini tunapaswa "*tafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake*"?

Kwa sababu ya ubora wake wenye thamani. Mat. 13:44-46, "*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile. Tena ufalme wa mbinguni umefanana na mfanya biashara mwenye kutafuta lulu nzuri; naye alipoona lulu moja ya thamani kubwa, alikwenda akauza alivyo navyo vyote, akainunua.*"

Ufalme wa mbinguni hakipaswi kuwa kitu tupu au ambacho hakina thamani kwetu. Fil. 3:8, "*Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo.*"

Paulo alikuwa na elimu na ujuzi wa jamii ya Kiyahudi. Aliihesabu kama mavi katika kazi yake kwa ajili ya Kristo.

Kwa sababu ya kipindi chake cha milele.

1 Yoh.2:16-17, "*Maana kila kilichomo duniani, yaani tama ya mwili, na tama ya macho, na kiburi cha uzima havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita pamoja na tama zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.*"

Kwa sababu huu ndio muda tulionao wa kuyapata. 2 Kor. 6:2, "*(Kwa maana asema wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama wakati uliokubalika ndio sasa; tazama siku ya wokovu ndio sasa.)*"

Kwa sabubu hatuna ahadi ya kesho.

Leo ndio wakati wetu wa kutumia na kuthibitisha; kesho ni ya Mungu na anaweza kuitoa au asiitoe.

- Mit. 27:1, "*Usijisifu kwa ajili ya kesho; kwa maana hujui yatakayozaliwa na siku moja.*"
- Yak. 4:13-15, "*Haya basi ninyi msemao leo au kesho tutaingia katika mji fulani na kukaa humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida; walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka. Badala ya kusema Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi.*"

Ametoa ahadi ya hisani – "*… na hivi vyote mtazidishiwa.*"

Kitu gani? Vitu ambavyo ni vya <u>msingi</u> viwezavyo kutusaidia katika maisha haya, kama chakula na nguo; sio vitu tunavyotamani.

Mat. 6:24-26, "*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali. Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je si zaidi ya chakula, au mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani, na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je si bora kupita hao?*"

Kama tukivitafuta vitu tunavyo vitamani, basi hatumtumikii Mungu.

Mat. 6:28-32, "*Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi wala hayasokoti nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama moja wapo loa hayo. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? Msisumbuke basi mkisema, tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote.*"

Bwana ameahidi ya kuwa atatupatia kila kitu <u>tunachokihitaji</u> katika maisha haya **<u>ikiwa</u>** tukitafuta kwanza "*ufalme wa Mungu na haki yake.*"

Ahadi yake inakikomo.

Waaminifu hakika wanaweza kubaatika kutimia kwa ahadi hii – "*… na hivi vyote <u>mta</u> zidishiwa.*"

Sivyo "labda hivyo" lakini "ata". Hiyo ndiyo ahadi yake.

2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.*"

Hii haimaanishi kwamba hii iliyopo ni rahisi kutengeneza maisha, bali inamaanisha kwamba hii iliyopo inatupatia njia ya uhakika wa kutengeneza maisha.

Mwisho

Je! Unatafuta kwanza ufalme wa Mungu?

Kama hapana, siyo kwamba tu utakosa kitu kikubwa katika maisha haya, bali pia utaikosa mbingu siku ya mwisho.

Tunafanya kazi na kujisikia tumechoka na kupata maumivu katika maisha haya. Bali kama tukiwa waaminifu na mara zote tunamuweka kuwa wa kwanza katika maisha yetu ndani ya maisha haya, Ameahidi kutujali katika maisha yajayo.

Ufu. 21:4, "*Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.*"